**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Simu:027-2553066
Nukushi: 027 - 2553245.
Barua pepe: patanditc@moe.go.tz

**Tovuti:** http://www.patanditc.ac.tz.

Chuo Cha Ualimu Patandi,
S.L.P 66,

Duluti,
**Arusha**

**NDUGU:……………………………………………..**

**YAH: MAELEKEZO KWA WANACHUO WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU ELIMU MAALUMU NGAZI YA STASHAHADA 2025/2026**

## 1. UTANGULIZI.

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu ngazi ya **Stashahada mwaka wa masomo 2025/2026.** Nakupongeza kwa kuchaguliwa kwako. Karibu sana. **Unatakiwa kuripoti Chuoni kuanzia tarehe………………….. hadi tarehe……………….. Kuchelewa kufika chuoni kutasababisha kupoteza nafasi yako ya kujiunga na chuo hiki.**

**Mahali chuo kilipo.** Chuo cha Ualimu Patandi kipo Kilomita **11.5** kutoka Arusha mjini katika eneo la Tengeru, kijiji cha Patandi kando kando ya Mlima Meru katika barabara kuu ya Arusha-Moshi-Dar-es-Salaam. Popote utakapotokea omba kushushwa katika kituo cha mabasi cha Tengeru ambapo utaona ukuta wa chuo. Geti la chuo lipo umbali wa mita 200 toka kituo cha magari.

**Vision:** To be a Center of Excellence in Promoting Special Needs Education and Inclusion worldwide by preparing teachers with specialized skills to meet the diverse needs of learners for equal access to quality education and become a leading institution aiming at fostering an inclusive society that values the education for all individuals.

**Mission:**To prepare quality Special Needs Education (SNE) and Inclusive Education (IE) teachers in educating vulnerable learners to become independent and supporting society on how to live with special needy children.

**MOTTO: LEAVE NO ONE BEHIND**

## MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

### a) MWALIMU TARAJALI (PRE-SERVICE)

Ili kuthibitisha kwamba wewe ndiye uliyechaguliwa kwa Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu, lazima uje na vitu vifuatavyo:-

i. Cheti halisi (Original Certificate na *kopi* zake 02) cha kufuzu mtihani wako wa Kidato cha nne na sita

ii. Nakala ya fomu ya kuitwa chuoni ('print'fomu/joining insruction hii)
iii. Fomu ya kuthibitisha hali ya afya yako iliyojazwa taarifa za ukweli na Daktari wa Hospitali ya Serikali (Wilaya/Mkoa). **(Fomu imeambatanishwa).**
iv. Cheti cha kuzaliwa (nakala 02 za vivuli vyake)
v. Unatakiwa kuja na kadi ya bima ya afya (NHIF) kutokana na umuhimu wake wa kurahisisha matibabu yako

**b) MWALIMU ALIYEHITIMU MAFUNZO YA UALIMU AMBAYE HAJAAJIRIWA**

Mahitaji yake ya kiusajili ni kama ya mwalimu kazini kasoro kigezo cha barua ya ruhusa kutoka kwa mwajiri na kitambulisho cha kazi.

**c) MWALIMU KAZINI**

**d)** Ili kuthibitisha kwamba wewe ndiye uliyechaguliwa kwa Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu, lazima uje na vitu vifuatavyo: -

i. Kitambulisho chako cha Kazi.
ii. Barua kutoka kwa Mwajiri ya kukuruhusu kuja kusoma (Release Letter original) na nakala 02 za vivuli vya barua hiyo
iii. Cheti cha kidato cha Nne na cha Ualimu (original Certificates) na nakala 02 za vivuli vya vyeti hivyo.
iv. Nakala ya fomu ya kuitwa chuoni ('print'fomu/joining insruction hii)
v. Fomu ya kuthibitisha hali ya afya yako iliyojazwa taarifa za ukweli na Daktari wa Hospitali ya Serikali (Wilaya/Mkoa). **(Fomu imeambatanishwa).**
vi. Cheti cha kuzaliwa (nakala 02 za vivuli vyake),
vii. Unatakiwa kuja na kadi ya bima ya afya (NHIF) kutokana na umuhimu wake wa kurahisisha matibabu yako

**TANBIHI:**

i. Mara ufikapo chuoni ripoti katika Ofisi ya Msajili/Mhasibu/Mwadili wa wanachuo kabla hujaenda mahali popote ukiwa na mahitaji yote yaliyoorodheshwa hapo juu.
ii. Hutasajiliwa bila kuonesha vifaa hivyo hapo juu.

**B. ADA**.

Ada ya Mafunzo kwa mwaka mmoja ni TShs. 450,000/= tu. Fedha hiyo inaweza kulipwa kwa mkupuo mmoja, au nusu yake kila mwanzo wa muhula. Malipo ya fedha ya ada yanafanyika kwa njia ya mfumo wa kielectroniki wa kiserikali *Government Electronic Payment Getway (GePG),* hivyo unashauriwa kufanya mawasiliano na Mhasibu wa chuo ili akupatie namba ya malipo ya serikali (***control number)*** na maelekezo zaidi kupitia namba za simu hizi;

**0754 269121/0781269121/0657269121**

**C: MICHANGO MBALIMBALI**

Unatakiwa kulipia benki michango ifuatayo kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapo chini, na hivyo kukabidhi stakabadhi ya malipo ya benki (pay-in-slip) mara unaporipoti chuoni;

| S.NA | MCHANGO | KIASI | MAONI |
|---|---|---|---|
| 1 | Serikali ya Wanachuo | 5,000/= | Kwa mwaka |
| 2 | **Huduma ya kwanza** | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 3 | Usafi na mazingira | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 4 | Usajili na kitambulisho | 20,000/= | Kwa mwaka wa kwanza tu. |
| 5 | Michezo | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 6 | Ulinzi | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 7 | Kukodisha godoro | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 8 | Bima ya Afya | 50,400/= | **Kwa mwaka kwa asiye na bima** |
| 9 | Ukarabati | 25,000/= | Kwa mwaka |
| | **Jumla ya michango yote** | **200,400/=** | |

**Fedha zote za michango zilipwe kwenye akaunti ya chuo Na. 0150685268200, jina la akaunti ni PATANDI T.C EXPENDITURE iliyoko katika benki ya CRDB.**

**MUHIMU**

- **Uje na Tsh, 15,000/=** tu kwa ajili ya Tisheti.
- Kila mwaka chuo hufanya mahafali ya kuwaaga wanaohitimu ambapo kila mwanachuo hutakiwa kushiriki katika shughuli hiyo kwa kuchangia Shilingi 15,000/= tu ili kufanikisha maandalizi ya maafali hayo.

**D. SARE YA CHUO**

Nguo fupi na za kubana **<u>haziruhusiwi.</u>**

**KWA WAVULANA/WANAUME**

i. Shati la mikono mirefu rangi ya maji ya bahari (light blue). Ni vema ukanunua mashati aina ya ***tomato light blue*** ili kuepuka utofauti wa muonekano wa rangi. Kama utashindwa kuipata huko, njoo ununue kwenye maduka ya huku Arusha/chuo.

ii. Suti nyeusi (Suruali zenye upana wa kutosha na koti zenye kitambaa cha kufanana), tai nyeusi na soksi nyeusi. Uje na sweta jeusi lenye kola ya V kwa ajili ya kujikinga na baridi.

iii. Viatu vyeusi vya ngozi (viwe vya kufunika miguu. NB: Viatu aina ya buti haviruhusiwi.

iv. Nguo za michezo T/shirt na bukta (rangi ya bluu), trucksuit rangi ya bluunyeusi (darkblue) na raba.

**TANBIHI:** suruali iliyoshonwa kwa mtindo wa 'modo' haitaruhusiwa kuvaliwa chuoni.


**KWA WASICHANA/WANAWAKE**

i. Shati la mikono mirefu rangi ya maji ya bahari (light blue). Ni vema ukanunua mashati aina ya tomato light blue ili kuepuka utofauti wa muonekano wa rangi. Kama utashindwa kuipata huko uliko, njoo ununue kwenye maduka ya huku Arusha/chuo.


ii. Suti nyeusi (sketi mshono wa box/Λ shape na koti zenye kitambaa cha kufanana), tai nyeusi na soksi nyeusi. Uje na sweta jeusi lenye kola ya V kwa ajili ya kujikinga na baridi.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi (viwe vya kufunika miguu) na vyenye kisigino kifupi.
iv. Nguo za michezo T/shirt rangi ya bluu), trucksuit rangi ya bluunyeusi (darkblue) na raba.

**TANBIHI**: kwa mtindo wa mashono ya suruali kwa wavulana na sketi kwa wasichana, angalia kiambatisho cha ushonaji wa sare hapo chini;


**PICHA 1: SKETI**



MFANO WA RANGI YA SHATI



**PICHA 2: SURUALI**



**SARE KWA AJILI YA WANACHUO WA KIKE WA KIISLAMU.**

i. Kwa wanachuo wa Kiislamu wanaruhusiwa kushona Hijab. Blauz inatakiwa ipite magoti na iwe pana (short kanzu) yenye rangi ya light blue (blue bahari). Kama utashindwa kupata aina ya rangi hiyo huko (tomato light blue) ni vema uje kununua kwenye maduka ya huku Arusha ili kuepuka utofauti wa muonekano wa rangi.
ii. Suruali nyeusi pana.
iii. Kitambaa cha kichwani kinapaswa kuwa cha rangi ya light blue aina ya tomato light blue

**3. MAVAZI MENGINE MUHIMU**

Mavazi unayotakiwa kuja nayo hapa chuoni ni yale ya heshima, yenye kuonyesha maadili ya Ualimu. Mavazi hayo yatakuwa yanavaliwa mara baada ya ratiba ya masomo darasani siku za mwisho wa juma na mapumziko ya sikukuu.

**ANGALIZO:** Kandambili ni marufuku kuvaliwa bwaloni, ofisini, darasani na kwenye mikutano yote ya Chuo. Aidha ukikutwa na vitu vilivyokatazwa hapo juu hautarudishiwa na adhabu kali zitatolewa.

**4. MAHITAJI MUHIMU KWA AJILI YA MALAZI NA CHAKULA**

Ili kufanikisha masomo yako na maisha yako kwa ujumla unapokuwa hapa, vifaa vifuatavyo ni vya lazima: -

i. Blanketi 1 na chandarua cha mbu rangi nyeupe pembe nne kwani eneo hili lina mbu wengi na baridi kali.
ii. Shuka jozi mbili rangi ya bluu bahari.
iii. Mto na foronya mbili za bluu bahari.
iv. Sahani, bakuli, kikombe, (**Visiwe vya plastiki**) na kijiko kwa ajili ya chakula.

v. Koti la mvua au mwamvuli.
vi. Gum boots.
vii. Ndoo za maji mbili (moja ya usafi na nyingine ya maji ya kunywa)

**5. MAHITAJI YA LAZIMA KWA AJILI YA TAALUMA**.

i. Daftari zisizopungua 10 (3 quire) na vifaa vya kuandikia.
*ii.* Rimu mbili kwa mwaka kwa ajili karatasi za kutolea vivuli (photocopy) ukubwa wa A4. Aina ya karatasi iwe mojawapo kati ya hizi zifuatazo: **Nopa Top**; **Golden Star**; **Rotatrim**; **Logic 700** au aina nyingineyo ili mradi ni ya kutolea photocopy**.** *{Tafadhali* ***usilete*** ***"Dublicating au Typing Papers"****}. Rim* itahitajika kila muhula wa masomo.
iii. Kila muhula, utatakiwa kuandaa zana za kufundishia ambazo zitakaguliwa na kupewa alama kama sehemu ya kozi yako.
iv. Kukamilika kwa kozi yako ni pamoja na kufanya Utafiti. Kazi hiyo **sharti** ikamilike na ikabidhiwe kwa Mkufunzi atakayekuwa anakusimamia kabla ya mtihani wa mwisho.

**6. MAAGIZO MUHIMU KWA AJILI YA AFYA YA MWANACHUO**

i. Chuo hakina zahanati. Matibabu yote yatafanyika kwenye Hospitali ya Wilaya iliyoko umbali wa mita 500 kutoka Chuoni.
ii. Unatakiwa kujiandalia akiba ya fedha kwa ajili ya matibabu pindi utakapoumwa. Hata hivyo, ili **kuepuka matatizo na usumbufu, mzazi unaelekezwa na unasisitizwa kumkatia bima ya afya mwanao, au kumpatia fedha ya kukatia** ***kadi ya bima ya afya mara atakapofika chuoni. Kadi ya bima ya afya ya NHIF ni shilingi 50,400/= tu. (Ni lazima kila mwanchuo kuwa na bima ya afya ya NHIF wakati wote akiwa masomoni).***
iii. Chuo **hakitoi** chakula maalumu (**special diet**). Iwapo una matatizo ya chakula ni vema ujiandalie fedha za kutosha kwa ajili hiyo

**NB:** Matatizo ya kiafya yasiyoelezwa katika Fomu ya matibabu, chuo hakitashughulikia changamoto zitokanazo na matatizo hayo. Hivyo unatakiwa kuwa mkweli. Aidha FOMU kwa ajili ya kupima afya imeonyeshwa katika (**KIAMBATISHO NA.1)**

**7. MAWASILIANO**

i. Taarifa zote muhimu kama maafa au msiba toka nyumbani zipitie kwa Mkuu wa Chuo na si kwa mwanachuo moja kwa moja.
ii. Unatakiwa kuwaelekeza ndugu zako kutoa taarifa kwa uongozi wa Chuo kuhusiana na tatizo la nyumbani na siyo kukutaarifu WEWE moja kwa moja.
iii. Barua zote za kuitwa au kualikwa kwenye vikao mbalimbali hazina budi zipitie kwa Mkuu wa Chuo.

**NB:** Taarifa itakayoletwa na mwanachuo haitasikilizwa.

**8. MENGINEYO.**

i. Kila mwanachuo anatazamiwa awe na mwenendo wa kiualimu na tabia nzuri wakati wote wa kozi yake.
ii. Kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za vyuo vya Ualimu mwanachuo, atalazimika kulala ndani ya Chuo na si Vinginevyo.
iii. Unatakiwa kushiriki kikamilifu katika Shughuli zote zinazoendeshwa Chuoni Hapa.
iv. Hereni, vidani, uwekaji wa madawa kwenye nywele (Relaxer, curl), kuvaa nywele za bandia (wig), kupaka wanja, kupaka rangi midomo na kucha,kufuga knywele ndefu au

kunyoa panki na kufuga ndevu na kuvaa nguo fupi zinazobana au kuangaza haviruhusiwi wakati wowote uwapo chuoni hapa.

v. Kipindi chote cha mafunzo mwanachuo wa kike haruhusiwi kubeba ujauzito,kuoa au kuolewa.

## 9. NGUZO/KANUNI NA TARATIBU ZA MWENENDO BORA CHUONI

i. Nidhamu inapewa kipaumbele katika kufanikisha taaluma na maadili bora ya kiualimu, hivyo unatarajiwa kuzingatia kanuni hizo ili uweze kuwa mwalimu uliye bora.

ii. Nguzo za Chuo zimeambatishwa; unatakiwa uzisome na kuzielewa. Iwapo unaona zitakuwia vingumu kuzifuata, ni heri ukate shauri kutokuja. Utakapofika Chuoni, utapewa maelekezo maalumu kuhusu Nguzo-Adili hizo.

**MWISHO:Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na watu wafuatao kwa namba zifuatazo;**

**Simu ya Mkuu wa Chuo 0767-275920 / 0716-767380**
**Simu ya Msajili 0625991519/0754991226/0622041727**
**Simu ya Mtaaluma 0759050839/0713589353**

Chuo kinakukaribisha sana Patandi, pamoja na kukutakia safari njema ya kufika hapa chuoni.
Pia fomu hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Elimu Sayansi na teknolojia**:** http:// www.moe.go.tz



Lucian Segesela

**MKUU WA CHUO**

CHUO CHA UALIMU PATANDI

**KIAMBATISHO NA 1.**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:**

From: Principal,
Patandi Teachers' College.
P. O. Box 66,
DULUTI.

TO: The Medical Officer

…………………………………… Name of student teacher
………………………………………..
………………………………………. ……………………………………

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time teacher's course.

A:1. (a) sickle cell
(b) Diabetes
(c) Venereal Diseases
(d) Leprosy
(e) Limbs
(f) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases.

B: Blood Group

Date: …………………….. Signature…………………………

Official Stamp

**************************************************************

**PART B:** **MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a full time teacher Education course.

(a) sickle cell…………………………………………………………
(b) Diabetes …………………………………………………………….
(c) Limbs…………………………………………………
(d) Speech……………………………………………………………….
(e) Leprosy……………………………………………………………….
(f) Neuroses………………………………………………………………………
(g) Other serious diseases…………………………………………………………..
(h) Pregnancy………………………………………………………………..

**Date…………………………………….…Signature……………………………**

**Official Stamp**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU ELIMU MAALUMU PATANDI**

# SHERIA ZA CHUO

Sheria hizi ni mwongozo wa namna ya kuishi na kuenenda ipsavyo kwa wanachuo wote wa chuo cha Ualimu Elimu Maalumu Patandi wawapo chuoni na nje ya Chuo. Hivyo ni lazima kwa mujibu wa sheria za Chuo kila mwanachuo kupata nakala ya sheria za Chuo. Aidha, mwanachuo anapaswa kuweka saini na kurudisha nakala ya sheria iliyosainiwa kwa Mwadili wa Wanachuo ili kuhifadhiwa kwenye kumbukumbu zake.

## 1. RUHUSA KWA WANACHUO:-

i. Ruhusa za siku kwa mwanachuo yeyote zitatolewa na Mkufunzi wa zamu kwa kibali cha maandishi.

ii. Ruhusa zote za kwenda kulala nje ya Chuo zitatolewa na Mkuu wa Chuo kupitia ofisi ya Uadili. Hivyo ni marufuku kwa mwanachuo kujiamulia kuondoka chuoni kwa muda mfupi au mrefu pasipo ruhusa/ kibali cha maandishi. Kulala nje ua Chuo bila kibali itapelekea mwanachuo kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kusimamishwa mafunzo au kuachishwa mafunzo.

iii. Ruhusa ya jumla kwa wanachuo kwa siku ya Jumamosi (kwa wanachuo wasio wa dhehebu la sabato) na sikukuu zisizo za kidini zitatolewa kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 10:30 jioni. Kwa siku ya Jumapili wanachuo wa dini ya kikristo) wasio wasabato wanatakiwa kwenda ibadani na wanachuo wote wanatakiwa kuwa wamerudi chuoni saa 10;30 jioni.

iv. Ni lazima kila mwanachuo kuwahi rollcall (mwitiko wa pamoja) saa 11:00 jioni kila Jumamosi, Jumapili na siku za sikukuu. Aidha kwa siku za kawaida mwanachuo hatakiwi kuwa nje ya Chuo baada ya saa 12:00 jioni.

v. Mwanachuo yeyote atakayekutwa katika mazingira ya chuo bila kibali cha maandishi juu ya uwepo wake kutoka Uongozi wa Chuo wakati angali akitumikia adhabu ya kusimamishwa Chuo kwa muda ikiwa haijakoma atakuwa ametenda kosa.

## 2. MATUMIZI YA VILEO NA MADAWA YA KULEVYA:

i. Hairuhusiwi Mwanachuo kutumia kilevi cha aina yeyote kama vile bangi, madawa ya kuelvya, mirungi, sigara, kuberi, ugoro na shisha ndani na nje ya chuo.

ii. Pia ni marufuku kwa mwanachuo kuonekana amelewa. Aidha ni kosa kwa mwanachuo kunywa au kupeleka pombe aina yeyote ya kilevi bwenini au darasani na maeneo yote ndani ya Chuo.

iii. Ni marufuku kwa mwanachuo awapo nje ya chuo kuonekana katika nyumba za wageni kama hayupo safarini au maeneo ya starehe ikiwemo bar, vilabu vya pombe, madanguro nk.

*Mwanachuo atakayebainika kutenda makosa haya atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kusimamishwa mafunzo au kuachishwa mafunzo au kupelekwa kwenye vyombo vya Dola.*

**3. UMILIKI WA SILAHA:-**

i. Ni kosa kwa mwanahuo yeyote kumiliki silaha au kushikilia zana ya kivita au kutumia kifaa chochote tofauti na matumizi yake na kupelekea kuhatarisha amani ya wanajamii. Iwapo mwanachuo atakuwa na kosa hilo atachukuliwa hatua stahiki za kinidhaamu kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo ikiwemo kupelekwa kwenye vyombo vya Dola.

ii. Mwanachuo atakayefanya vitendo vitakavyosababisha kushambulia,kufanya tishio la kudhuru mtu mwingine au kujidhuru mwenyewe, katika mazingira ya Chuo, mwanachuo huyo atachukuliwa hatua za kinidhamu/ kisheria kadri yake.

**4. USAFI, AFYA NA MAVAZI:-**

i. Wakati, wote ndani na nje ya Chuo, mwanachuo anatakiwa kuvaa mavazi yenye nidhamu, safi na yenye haiba ya kiualimu kulingana na mwongozo wa mavazi.

ii. Sare ya Chuo itavaliwa wakati wote wa vipindi au mwanchuo anapotoka nje ya chuo. mavazi mengine yaliyokubaliwa chuoni (Mfano Tshrts, trucksuit na nguo za michezo zingine) yatavaliwa kwa mujibu wa ratiba na mwongozo wa chuo uliopo.

iii. Hairuhusiwi kwa mwanachuo kuvaa kaptula, malapa, nguo za mipasuo inayovuka magoti, sketi fupi kuvuka magoti, suruali za kubana (Modal), kuvaa mlegezo na kofia Pamoja na nguo zozote zisizofaa kwa mwanachuo wa kiume na kike kadri yake.

iv. Ni marufuku kwa mwanachuo kuwa na nywele zisizo punguzwa (ndefu) au zisizotunzwa vizuri. Mwanachuo pia haruhusiwi kuacha kucha ndefu na zilizowekwa rangi, kufuga ndevu, kunyoa panki kadiri yake. Mwanachuo anatakiwa kutunza meno yake vizuri na kinywa. Wasichana wanaruhusiwa kusuka nywele zao lakini haiuruhusiwi kutumia kemikali katika nywele na ngozi au kubadilisha rangi ya nywele pamoja na kusuka nywele za rangi au rasta.

v. Ni marufuku kwa mwanachuo kupeleka chakula bwenini. Chakula chote kitaliwa bwaloni au canteen, isipokuwa kwa idhini maalumu kutoka ofisi ya uadili.

*Mwanachuo atakayebainika kuwa na makosa hayo atachukuliwa hatua staiki za kinidhamu. **Tanbii:** Chuo hakitoi chakula maalumu*.

vi. Mwanachuo haruhusiwa kutoa mimba, kushawishi au kumsaidia mwanchuo mwingine kutoa mimba. Mwanachuo atakayebainika kufanya kitendo hicho, atachukuliwa hatua stahiki za kinidhamu na kisheria.

5. **TAALUMA:-**

i. Mwanachuo anapaswa kuhudhuria darasani vipindi vyote vya masomo kulingana na ratiba kwa kipindi chote cha mafunzo.

ii. Mwanachuo anapaswa kuwa na vifaa vyote vya kujifunzia ikiwemo madaftari kalamu na vingine vitakavyokuwa vimeagizwa na ofisi ya taaluma au idara za masomo.
iii. Mwanachuo anapaswa kufanya kazi binafsi, majaribio na mitihani yote kulingana na miongozo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Chuo.
iv. Mwanachuo anapaswa kushiriki katika clubs za masomo, makongamano ya kitaaluma na siku za watu wenye ulemavu kulingana na ratiba ya chuo.
v. Mwanachuo anapaswa Kushiriki masomo ya jioni (prepo) katika kipindi chote cha mafunzo.

**Adhabu:**

i. Kushindwa kuhudhuria vipindi darasani bila sababu mwanachuo anaweza kupewa adhabu, kusimamishwa mafunzo kwa siki 14 au 21 au kuachishwa mafunzo kwa mujibu wa sharia na taratibu.
ii. Mwanachuo kushindwa kuwa na vifaa vyote muhimu vya kujifunzia hatasajiliwa au kuruhusiwa kuingia darasani.
iii. Kufanya vitendo vya kugushi au udanganyifu wakati wa kazi za vikundi, majaribio na mtihani, kutapelekea mwanachuo atakayebainika kufutiwa matokeo yake yote.
iv. Kutokufanya kazi za vikundi, kazi binafsi, majaribio na mtihani bila sababu, mwanachuo husika anaweza kupewa adhabu/kusimamishwa masomo kwa siku 7 au 14.
v. Kutokushiriki clubs za masomo, kujisomea muda wa jioni vipindi vya dini kutapelekea mwanachuo kupewa adhabu.

6. M**ASUALA YA USAWA WA KIJINSIA NA UJUMUISHI(UKU): -**

Unyanyasaji wa kijisia au wa kimaumbile na ubaguzi wa aina yoyote haukubaliki chuoni.

Vitendo hivyo ni kama: -

i. Kumlazimisha mtu kwa kumtaka kimapenzi kwa kutumia maneno, ishara, picha au vitisho vyenye maudhui ya kimapenzi au kufanya vitendo, au kutumia lugha inayosababisha mtu mwingine kukosa amani ama kushindwa kuendelea na masomo/kazi yake au kujisikia vibaya kutokana na hali yake na maumbile yake.
ii. Hairuhusiwi kwa mwanachuo kuandika au kuchora picha zinazoashiria matusi, kejeli au udhalilishaji wa mtu mwingine yeyote ndani na nje ya Chuo. Kwa njia yeyote ile.

Kwa mwanachuo au mtu yeyote atakayepatikana na kuthibitika kuhusika na vitendo vya aina hiyo, atachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa kanuni, sheria na taratibu na miongozo iliyopo.

**7. ULINZI NA USALAMA: -**

i. Kila mwanachuo ni lazima kuwa mlinzi wa mali zake, za wenzake na za umma.

ii. Mwanachuo akipoteza au kuharibu mali ya chuo au ya mtu mwingine, atachukuliwa hatua za kinidhamu/sheria ikiwa ni Pamoja na kulipa gharama za mali husika.
iii. Wizi wa mali ya mwingine au mali ya umma itapelekea mwanachuo kuchukuliwa hatua za kinidhamu/ sheria ikiwemo kusimamishwa mafunzo au kuachishwa mafunzo Pamoja na kurejesha kitu hicho kwa gharama yake.
iv. Ni kosa kwa mwanachuo kufanya vitendo vinavyohatarisha usalama au kuleta hasara kwa watu au chuo, kwa mwanachuo atakaye tenda kosa hilo hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kusimamishwa masomo.
v. Mwanachuo anapaswa kujiepusha na vitendo vya utapeli na kujipatia mali au manufaa mengine kwa njia ya ulaghai, na isiyohalali. Akibainika kufanya hivyo, hatua za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kusimamishwa au kuachishwa mafunzo.
vi. Hairuhusiwi kuhamisha samani za chuo, (viti na meza) kutoka sehemu moja Kwenda sehemu nyingine bila ya kibali kutoka kwa mlezi husika.
vii. Ni marufuku kwa mwanachuo kuandika maandishi yoyote katika majengo au katika vifaa mablimbali. Kwa mwanachuo atakayetenda kosa atachukuliwa hatua stahiki za kinidhamu.
viii. Ni kosa kufanya matumizi mabaya na hatarishi ya umeme katika Chuo cha Ualimu Patandi. Matumizi ya mishumaa, chemli, na jiko la umeme/gesi, heater, au birika za umeme. Mwanachuo atakayebainika na makosa haya atachukuliwa hatua za kinidhamu Pamoja na kunyang'anywa vifaa hivyo na kulipa gharama za hasara itakayopatikana.

**8. MAHUSIANO YA KIMAPENZI, UBAKAJI, ULAWITI USAGAJI NA USHOGA: -**

i. Ubakaji, ulawiti, usagaji na ushoga haviruhusiwi katika chuo na mahali, pengine popote ndani na nje ya Chuo. Mwanachuo atakayebainika kujihusisha na vitendo hivyo, atachukuliwa hatua stahiki za kinidhamu ikiwemo kusimamishwa mafunzo, kuachishwa mafunzo au kupelekwa kwenye vyombo vya dola kadiri yake.
ii. Ni kosa kwa mwanachuo kuonyesha kwa njia yeyote ile kujihusisha na vitendo vya umalaya, uzinzi na uasherati, au kuonekana kuishi kama mtu na mpenzi wake au mume na mke katika maisha yake hapa chuoni.
iii. Mwanachuo haruhusiwi kuoa au kuolewa awapo chuoni katika kipindi chote cha mafunzo
iv. Mwanachuo haruhusiwi kupata ujauzito au kumpa ujauzito mwanachuo mwenzake au mtu mwingine wakati wote wa kipindi cha mafunzo.

Mwanachuo atakayebainika kujihusisha na vitendo hivyo hapo juu (ii, iii, na iv), atachukuliwa hatua stahiki za kinidhamu Pamoja na kupewa ushauri mbadala kadiri yake.

**9. HESHIMA NA UTII: -**

i. Kila mwanachuo ajiheshimu kwa kuweka mwili wake na mavazi yake katika hali ya usafi na heshima.
ii. Awe na lugha yenye staha na hadhi ya Ualimu na matendo yake yawe yanakuza heshima ya Ualimu.
iii. Kila mwanachuo awe na utii kwa viongozi wa Serikali ya wanachuo(SEWAPA), walezi wake, Uongozi wa Chuo na mamlaka zingine ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
iv. Ni kosa kwa mwanachuo kutotekeleza adhabu au maelekezo aliyopewa na viongozi wa SEWAPA, walezi au mamlaka ya chuo.
v. Kila mwanachuo anapaswa kuwa mtiifu kwa kengele au ishara yoyote itakayomuhitaji kufika mahali panapo takiwa.
vi. Ni marufuku kwa mwanachuo wa kike au wakiume kutembelea bweni la jinsi nyingine bila ruhusa au kibali maalumu kutoka kwa mkufunzi wa zamu, mwadili, matroni au patroni.
vii. Kila mwanachuo anapaswa kuwa na mazoea ya kusalimia, kusimama kwa heshima pale anapopita mkubwa na kupokea mzigo kwa mkubwa wake, viongozi na walezi
viii. Mwanachuo hapaswi kuwa na matumizi ya lugha ya matusi, kejeli au kutishia zinazofanya na mwanachuo dhidi ya wanachuo wenzake, walezi wake au mtu yeyote wa ndani au nje ya chuo.
ix. Mwanachuo atakayebainika kutokuzingatia vitendo vinavyoonesha heshima na utii atachukuliwa hatua za kinidhamu.

**10. UCHOCHEZI: -**

i. Mwanachuo hairuhusiwi kushiriki au kuchochea, kushawishi, migomo ya aina yoyote au maandamano wakati wowote awapo Chuoni
ii. Wakati wote mwanachuo atatakiwa kutumia busara na hekima katika kutatatua changamoto au migogoro chuoni na mahali pengine popote. Hii ni Pamoja na mwanachuo kutumia vikao halali na vyombo/ mifumo ya mawasiliano iliyowekwa chuoni kuwasilisha n akutatua changamoto zake.

Mwanachuo atakayebainika kujihusisha na vitendo vya na i. na ii hapo juu atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwemo kusimamishwa mafunzo au kuachishwa mafunzo.

**11. MIKUTANO NA MAWASILIANO CHUONI: -**

i. Mwanchuo anapaswa kuhudhuria mikutano yote iliyopangwa na Chuo
ii. Mikutano mingine yoyote ya wanachuo chuoni, lazima ofisi ya Uadili ifahamishwe kabla ya kufanyika. Tafrija, video, disko, mikutano ya dini, vikao

vya Serikali ya wanachuo nk vinaingia katika fungu hili. Si ruhusa kuitisha mkutano bila kibali.

iii. Taarifa zinazomhusu mwanachuo kutoka nyumbani kwao mfano zinazohusu msiba ugonjwa nk. Ni lazima zipitie kwa Mkuu wa Chuo ikiwemo ofisi ya uadili au Makamu Mkuu wa Chuo.

iv. Mwanachuo atapaswa kueleza habari za kweli pale atakapotakiwa na mamlaka ya chuo kufanya hivyo. Ni kosa kwa mwanchuo kutoa taarifa za uongo au kuficha siri/taarifa ya kutendeka kwa kosa au uhalifu wowote, ikidhihirika hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mwanachuo huyo.

v. Wasemaji wa mambo ya wanachuo kwa uongozi wa chuo ni serikali ya wanachuo

vi. Ni kosa kwa mwanachuo yeyote kutoa taarifa za chuo kwa mtu yeyeote au kupeleka taarifa za chuo kwenye vyombo vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii (radio, TV, magazeti nk) bila kibali cha Mkuu wa Chuo. ***Ikumbukwe kuwa msemaji wa chuo kuhusu masuala mbalimbali yahusuyo Chuo ni Mkuu wa Chuo***. Hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa yeyote atakayebainika kukiuka misingi na taratibu za Chuo. Ikumbukwe msemaji Mkuu wa chuo ni Mkuu wa Chuo.

vii. Mwanachuo haruhusiwi kutumia mitandao ya mawasiliano kinyume na sheria za mitandao zilizowekwa na mamlaka husika (TCRA). Mwanachuo akibainika kufanya hivyo hatua za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

viii. Mwanachuo haruhusiwi kutembelea nyumba za Watumishi bila kibali cha Mkufunzi wa zamu na ofisi ya Uadili.

ix. Wageni wa wanachuo wataruhusiwa kuwatembelea wanachuo siku ya Jumamosi au Jumapili kuanzia saa 5:00 asubuhi na mwisho wa kuwepo chuoni nis aa 11:00 jioni. Mwanachuo anapaswa kutoa taarifa ya mgeni wake ofisi ya Uadili au mkufunzi wa zamu. Hairuhusiwi mgeni wa mwanachuo yeyote kupelekwa bwenini.

x. Mwanachuo haruhusiwi kuwabughubudhi wanachuo wenzake kwa makelele ya aina yeyote ileikiwemo mayowe na miziki.

*Mwanachuo atakayebainika kutenda makosa yaliyobainishwa atachukuliwa hatua za kinidhamu.*

## 12. SHERIA ZA NCHI:-

i. Kila Mwanachuo ni lazima kuzitii na kuzifuata sheria za Nchi na alama za Taifa.
ii. Ni kosa la kijinai kwa mwanachuo kughushi vyeti au kufanya udanganyifu mwingine unaompa sifa za kitaaluma. Ukibainika utaachishwa mafunzo na kushitakiwa mahakamani
iii. Ni kosa kwa mwanachuo kujihusisha na mambo ya siasa awapo Chuoni. Hii ni kutokana na Chuo kuwa Taasisi ya Serikalin a hivyo hakifuati itikadi yoyote ya kisiasa.

*Kila mwanachuo anafahamu kuwa mwanachuo sio kigezo cha kutotii sheria za Nchi.*

13. Kwa mwanachuo ambaye ni mwajiriwa wa Serikali chini ya masharti ya utumishi wa Umma (Ualimu) TSD kanuni zinazotawala maadili ya ualimu zitazingatiwa.

**TAMKO LA MWANACHUO MUHUSIKA**

Mimi ______________________________ nimezisoma sheria za chuo cha Ualimu Elimu Maalumu Patandi na kuzielewa. Baada ya kuzisoma na kuzielewa, naahidi kuishi kwa kuzifuata kwa muda wote nitakaokaa hapa Chuoni/ Nimeona nitashindwa kuziishi na kuzifuata sheria hizi na hivyo naomba kuahirisha mafunzo haya.

Tarehe ___________________ saini___________________________



Lucian E. Segesela

**MKUU WA CHUO**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU PATANDI